

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA TANO

28 APRILI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 28 APRILI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

185. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza madarasa katika Shule ya Msingi Puma kutokana na kuzidiwa na idadi ya Wanafunzi.

**186. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule ya Kidato cha Tano na Sita katika Jimbo la Tunduru Kusini.

**187. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO
(SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, mpango wa kutumia majengo ya Sekondari ya Sengerema kuwa Chuo cha Madini na Uvuvi umefikia wapi.

**188. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA
(MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mkato kati ya Wilaya za Mbarali na Chunya ili kupunguza gharama za usafiri na kukuza biashara.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

189. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni kesi ngapi za Wakulima kulishiwa mazao yao zimeripotwa na ngapi zimepelekwa Mahakamani.

WIZARA YA AFYA:

190. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali haioni haja ya kuupitia tena Muundo wa Utumishi wa Madaktari Bingwa wa Mwaka 2022.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

191. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa kodi kwenye Vifaa vinavyotumiwa na Watu wenye Ulemavu wakati wa kuingia nchini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

192. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati kwenye Vyuo Vikuu vyenye miundombinu chakavu.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

193. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini mpaka wa Kasesya/Zombe utafanya kazi kwa ufanisi ili kupunguza msongamano wa malori katika mpaka wa Tunduma.

194. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja litakalounganisha Tanzania Bara na Zanzibar.

**195. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA
(UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni ni busara kuuza nyumba kwa Wapangaji wa kota za Ukonga kwa kuwa wameishi miaka mingi bila kufanyiwa ukarabati.

WIZARA YA KILIMO:

**196. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA
(KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kusaidia kuongezeka kwa bei ya Zao la Chai kwa Wakulima nchini.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**197. MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR
(GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mkakati gani wa kuandaa Filamu zenye kueleza Historia ya Nchi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
28 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

